TANGAZO LA SERIKALI NA. 333 la Tarehe 20/07/2018

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA

SURA 290

# SHERIA NDOGO

*Zimetungwa chini ya vifungu vya 6(1) na 16(1)*

SHERIA NDOGO (ADA NA USHURU) ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA KIGAMBONI ZA MWAKA, 2018

Jina na mwanzo wa kuanza kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni za mwaka, 2018 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililo chini ya mamlaka ya Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakapoelekezwa vinginevyo:-

*"Ada na Ushuru"* maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri kwa ajili ya huduma, vibali, au leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri;

*"Afisa masuuli"* maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri au Afisa yeyote atakaye idhinishwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

*"Afisa Mwidhiniwa"* maana yake ni Afisa yeyote aliyeteuliwa na Halmashauri kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

*"Halmashauri"* maana yake ni Halmashauri ya Manispaa Kigamboni;

*"Kibali'* maana yake ni idhini au ruhusa ya maandishi inayotolewa na Halmashauri;

*"Leseni"* maana yake ni kibali cha maandishi kinachotolewa kwa Mtu binafsi, Kampuni au taasisi kinacho ruhusu kufanya biashara au shughuli yoyote katika eneo la Halmashauri;

*"Machinjio"* maana yake ni sehemu iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuchinjia wanyama na kuanika ngozi;

*"Masoko"* maana yake ni maeneo maalumu iliyotengwa na kumilikiwa na Halmashauri kwa ajili ya biashara ya kuuza na kununua bidhaa au huduma kufuatana na taratibu zilizowekwa na Halmashauri;

*"Mazao ya bahari"* maana yake ni viumbe vyote hai na visivyo hai ambavyo hupatikana katika bahari;

*"Mkurugenzi"* maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa Kigamboni pamoja na Afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

*"Mkataba"* maana yake ni makubaliano yenye nguvu ya kiSheria ya ununuzi au uuzaji au utoaji wa huduma yo yote kati ya Halmashauri na wadau wa Halmashauri;

*"Ushuru wa Madini ya Ujenzi"* maana yake ni Ushuru utakaotozwa kwa kibali cha uchimbaji wa Kokoto, Mawe, Changarawe, Mchanga, Chokaa, Marumaru, Kifusi, Udongo Mfinyanzi au chochote kinachochimbwa katika Mamlaka ya Halmashauri kwa shughuli za ujenzi;

*"Wakala"* maana yake ni Mtu, Taasisi, Kampuni au asasi yoyote iliyoteuliwa kisheria na Halmashauri kukusanya mapato kwa niaba ya Halmashauri;

Ada na Ushuru

4. (1) Halmashauri itatoza Ada na Ushuru katika biashara, huduma, vibali, au leseni mbalimbali zinazotolewa na Halmashauri kama ilivyoorodheshwa kwenye Jedwali la kwanza Sheria Ndogo hizi.

(2) Bila kuathiri masharti ya jumla kifungu kidogo cha (1 ) cha 4 cha Sheria Ndogo hizi, Halmashauri itatoza Ada na Ushuru katika vyanzo vifuatavyo:-

i. Ukodishaji wa mitambo ya Halmashauri;
ii. Ushuru wa viwanda vya matofali;
iii. ushuru machinjio na mnada;
iv. ushuru wa samaki na mazao ya bahari;
v. ushuru wa mazao;
vi. ushuru wa mazao ya baharini;
vii. ada ya maombi ya kujenga vituo vya kuoshea magari;
viii. ada za maombi ya zabuni mbalimbali za Halmashauri;
ix. ushuru wa kuegesha vyombo vya usafiri majini;
x. Ada za upimaji ardhi;
xi. Ada ya Vibali vya ujenzi na Uhakiki wa Vibali vya ujenzi;
xii. ada za matumizi ya fukwe za bahari;
xiii. Ushuru wa madini ya ujenzi.

Namna ya kukusanya Ada na Ushuru

5 (1) Halmashauri itaweka utaratibu itakavyoona inafaa ikiwa ni pamoja na kutenga maeneo maalum ya kutoza Ada na Ushuru kutoka vyanzo vya mapato kama ilivyoainishwa kwenye kifungu kidogo cha (2) cha kifungu cha 4 cha Sheria Ndogo hizi.

(2) Malipo ya Ada au Ushuru yanayotozwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi yatalipwa kwa Halmashauri au wakala na kutolewa stakabadhi halali ya kielektroniki kama kielelezo cha malipo yaliofanyika.

(3) Ada na Ushuru unaotozwa chini ya Sheria Ndogo hizi utalipwa kabla ya kupata huduma, leseni au kibali husika.

(4) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu cha 5 cha Sheria Ndogo hizi Halmashauri au wakala kwa idhini ya Afisa Masuuli itatoa kwa mlipaji stakabadhi halali ya kawaida kama kielelezo cha malipo yaliyofanyika.

(5) Halmashauri au Wakala atakuwa na mamlaka ya kukamata bidhaa au mali ya mtu yeyote endapo ameshindwa kulipa Ada au Ushuru ndani ya muda aliotakiwa kulipa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

(6) Endapo bidhaa au mali iliyokamatwa na Halmashauri au wakala haitalipiwa Ushuru unaodaiwa ndani ya siku 7 kwa mali au bidhaa zisizoharibika haraka, na ndani ya siku 2 kwa mali au bidhaa zinazoharibika haraka. Halmashauri itakuwa na uwezo baada ya kupata idhini au bila idhini ya mahakama kuuza bidhaa au mali na fedha zitakazopatikana Halmashauri itakata pesa inayodaiwa na kiasi kinachobakia atarudishiwa mmiliki.

Wajibu wa kulipa Ada au Ushuru

6 (1) Ni wajibu wa kila mtu anayetakiwa kulipa Ada au Ushuru kulipa kiwango cha Ada au Ushuru kama ilivyoainishwa kwenye Sheria Ndogo hizi.

(2) Ni wajibu kwa kila mtu kutoa taarifa sahihi kwa Halmashauri au Wakala kuhusu bidhaa au mali zinazotakiwa kulipiwa Ada au Ushuru.

(3) Itakuwa ni wajibu kwa kila mtu atakayelipa Ada au Ushuru kutunza kumbukumbu za malipo.

Kibali au leseni

7. (1) Halmashauri itatoa kibali au leseni kwa mfanyabiashara au mtu yeyote kwa kadri itakavyoona inafaa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

(2) Ni wajibu kwa kila mfanyabiashara au mtu yeyote anayetaka kufanya jambo lolote linalohitaji kibali au leseni kuomba na kupata leseni au kibali kutoka Halmashauri.

Ushuru wa Hoteli

8. (1) Kila mmiliki wa nyumba ya kulala wageni anapaswa kulipa asilimia kumi (10%) ya mapato yake kwa Halmashauri ambapo biashara hiyo inafanyika au kulipa kutokana na makubaliano kati ya mmiliki wa nyumba ya wageni na Halmashauri.

(2) Mmiliki wa nyumba ya kulala wageni anawajibika kuwasilisha taarifa za mauzo ya mwezi kwa Halmashauri ndani ya siku saba (7) tangu kumalizika

kwa mwezi wa malipo.

Uteuzi wa wakala

9. Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuteua Kampuni au Taasisi iliyosajiliwa kwa mujibu wa Sheria kukusanya Ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

Wajibu wa wakala

10. Wakala aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 9 cha Sheria Ndogo hizi atakuwa na wajibu wa:
(a) Kukusanya na kupokea Ushuru kwa niaba ya Halmashauri katika eneo alililopangiwa na kwa kiwango kilichoidhinishwa chini ya Sheria Ndogo hizi.
(b) Wakala atakusanya Ada au Ushuru kwa kutumia mfumo wa kielektroniki na kuwasilisha makusanyo yote kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala alioingia na Halmashauri.

Makosa kwa Wakala

11. Itakuwa ni kosa kwa Wakala kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi endapo:-
(1) atashindwa, atadharau, atakwepa au atakataa kulipa Ada au Ushuru au kutekeleza agizo lolote alilopewa na halmashauri kwa mujibu wa sheria Ndogo hizi.
(2) atamshawishi mtu au kundi la watu kukataa au kukwepa kulipa Ada au Ushuru.
(3) atamzuia kwa namna yoyote ile Afisa mwidhiniwa kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.
(4) atatumia nyaraka za kughushi kwa nia ya kujipatia manufaa yatokanayo na ukusanyaji wa Ada au Ushuru ndani ya halmashauri
(5) atashindwa au atatoa taarifa za uongo kwa Halmashauri au wakala kuhusu bidhaa au mali zinazotakiwa kulipiwa Ada au Ushuru.
(6) atashindwa kutunza kumbukumbu sahihi za malipo ya Ada au Ushuru.

Uwezo wa Afisa mwidhiniwa

12. Bila kuathiri masharti yaliyowekwa na Sheria Ndogo hizi Afisa Mwidhiniwa anaweza kuingia katika eneo lolote au jengo lolote kwa nia ya kukusanya au kufanya tathimini au kufanya jambo lolote linalohusiana na Ada, Ushuru, leseni au Kibali kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

Makosa

13. Itakuwa ni kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi iwapo mtu yeyote:-
(1) Atashindwa au atadharau au atakwepa au atakataa kulipa Ada au Ushuru.

(2) Atakataa au kushindwa kutekeleza agizo lolote atakalopewa na Halmashauri kupitia afisa wake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

(3) Atafanya jambo lolote linalotakiwa kulipia Ada au Ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi bila kulipia Ada au Ushuru.

(4) atamshawishi mtu au kundi la watu kukataa au kukwepa kulipa Ada au Ushuru.

(5) atamzuia kwa namna yoyote ile Afisa Mwidhiniwa kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

(6) atatumia nyaraka za kughushi kwa nia ya kujipatia manufaa yatokanayo na ukusanyaji wa Ada au Ushuru ndani ya Halmashauri.

(7) atashindwa kutoa taarifa sahihi au atatoa taarifa za uongo kwa Halmashauri au wakala kuhusu bidhaa au mali zinazotakiwa kulipiwa Ada au Ushuru.

(8) atashindwa kutunza kumbukumbu sahihi za malipo ya Ada au Ushuru.

(9) kufanya biashara yoyote bila ya kuwa na leseni pale ambapo biashara inayofanyika inahitaji kuwepo na leseni.
kuuza au kununua mifugo nje ya eneo la mnada

(10 kufanya biashara katika eneo lisiloruhusiwa;

(11 kuleta au kusababisha fujo kwenye mnada au katika eneo lolote ambalo maafisa au watumishi wa Halmashauri au mawakala wake watakapokuwa wakitekeleza majukumu yao;

(12 kujenga au kukarabati jengo lolote bila kuwa na kibali cha ujenzi hai kutoka Halmashauri;

(13 kutokuwa na nakala ya kibali cha ujenzi kwenye eneo la ujenzi wakati ujenzi ukiwa unaendelea.

Mamlaka ya kufunga biashara

14. (1) Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kufunga biashara yoyote ambayo mmiliki wake ameshindwa au kukataa kulipa Ada au Ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

(2) Halmashauri haitawajibika kwa hasara atakayopata

mtu au mfanyabiashara au taasisi yoyote kutokana na kutekeleza Sheria Ndogo ya 14(1) ya Sheria Ndogo hizi.

Kufifilisha Makosa

15. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza faini mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria hizi, kiasi kisichopungua shilingi laki mbili (Tsh.200,000/=) na kisichozidi shilingi laki tano (500,000/=) iwapo mkosaji atakiri kosa kwa hiari na kuwa tayari kujaza fomu maalum iliyoambatishwa kwenye Jedwali la pili la Sheria Ndogo hizi, na atatakiwa kulipa Ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

Adhabu

16.(1 Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa, na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi laki mbili (Tsh.200,000/=) na isiyozidi shilingi milioni moja (1,000,000/=) au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kuzidi miezi ishirini na nne au adhabu zote mbili kwa pamoja.

(2) Pamoja na adhabu atakayopewa mkosaji katika Sheria Ndogo hizi atawajibika kuilipa Halmashauri gharama iliyoingia kutokana na kuvunja masharti ya Sheria Ndogo hizi ikiwa ni pamoja na kulipa Ushuru anaodaiwa, gharama za kumkamata mkosaji na gharama za kukamata na kuhifadhi mali.

JEDWALI LA KWANZA

*Limetungwa Chini Ya Kifungu Cha 4 (1)*

SEHEMU YA KWANZA

UKODISHAJI WA MITAMBO YA HALMASHAURI

| | *Aina ya tozo* | *kiasi cha tozo* |
|---|---|---|
| 1. | Kukodi Grader | Tshs 850,000/= kwa siku |
| 2. | Kukodi Wheel Loader | Tshs 500,000/= kwa siku |
| 3. | Kukodi Bulldozer – D8 | Tshs 1,200,000/= kwa siku |
| 4. | Kukodi Bulldozer – D4 | Tshs 800,000/= kwa siku |
| 5. | Kukodi Cesspit Emptier Vehicle | Tshs 200,000/= kwa siku |
| 6. | Kukodi medium excavator | Tshs 600,000/= kwa siku |
| 7. | Kukodi Dump truck | Tshs 150,000/= kwa siku |
| 8. | Mitambo Mingine | Tshs 1,000,000/= kwa siku |
| 9. | Kukata barabara ya Halmashauri | Tshs 10,000,000/= |

SEHEMU YA PILI

USHURU WA VIWANDA VYA MATOFALI

Katika Maeneo yanayomilikiwa na Halmashauri Tshs 200,000/= Kwa Mwaka

SEHEMU YA TATU

1. ADA ZA MACHINJIO NA MNADA

A. Ada za machinjio kwa kila kichwa cha mfugo

| | | |
|---|---|---|
| I. | Ng'ombe | Tshs 5,000/= |
| II. | Mbuzi/Kondoo | Tshs 3,000/= |
| III. | Nguruwe | Tshs 3,000/= |

B. Ada za Ukaguzi wa mifugo

| | | |
|---|---|---|
| I. | Ng'ombe | Tshs 1,000/= |
| II. | Mbuzi/Kondoo | Tshs 500/= |
| III. | Nguruwe | Tshs 500/= |

C. Ushuru wa mifugo Mnadani kwa kila kichwa cha mfugo

| | | |
|---|---|---|
| I. | Ng'ombe | Tshs 3,000/= |
| II. | Mbuzi/kondoo | Tshs 1,500/= |
| III. | Nguruwe | Tshs 1,500/= |

D. Ada za leseni za Eneo, Uchunaji wa ngozi na Upangaji wa madaraja

| | | |
|---|---|---|
| I. | Ada ya leseni uchunaji na upangaji madaraja | Tshs 20,000/= kwa mwaka |
| II. | Ada ya Leseni ya Eneo | Tshs 50,000/= kwa mwaka |

SEHEMU YA NNE

2. USHURU WA SAMAKI NA MAZAO MENGINE YA BAHARI

| | |
|---|---|
| | Asilimia Tano (5%) ya bei ya mauzo |

SEHEMU YA TANO

3. USHURU WA MAZAO

| *NA.* | *AINA YA MAZAO* | *USHURU (Tsh)* |
|---|---|---|
| 1 | Mazao ya chakula | Asilimia 3% ya bei ya kununulia |
| 2 | Mazao ya biashara | Asilimia 3% ya bei ya kununulia |

SEHEMU YA SITA

ADA YA MAOMBI YA KUJENGA VITUO VYA KUOSHEA MAGARI

| | | |
|---|---|---|
| I. | Maeneo ya katikati ya Manispaa | Tshs 200,000/= kwa mwezi |
| II. | Nje ya maeneo ya katikati ya Manispaa | Tshs 100,000/= kwa mwezi |
| III. | Maeneo mengine | Tshs 50,000/=kwa mwezi |

SEHEMU YA SABA

ADA ZA MAOMBI YA ZABUNI MBALIMBALI ZA HALMASHAURI

| | | |
|---|---|---|
| I. | Ukusanyaji wa mapato | Tshs 100,000/= |
| II. | Ujenzi wa barabara | Tshs 100,000/= |
| III. | Ukusanyaji na uondoshaji wa taka ngumu | Tshs 50,000/= |
| IV. | Kupakua mashimo ya maji machafu (vyoo) | Tshs 100,000/= |
| V. | Kukarabati na kujenga vyoo vya uma, maduka Vioski na vizimba | Tshs 70,000/= |
| VI. | Kurekebisha mali za Halmashauri (magari na majengo) | Tshs 100,000/= |
| VII. | Ukaguzi na upimaji wa viwanja. | Tshs 100,000/= |
| VIII. | Uendeshaji vyoo vya umma Tshs | Tshs 100,000/= |
| IX. | Uendeshaji wa vioski vya Halmashauri | Tshs. 50,000/= |
| X. | Huduma elekezi / mshauri (Consultancy services) | Tshs. 100,000/= |
| XI. | Upangishaji Maduka / Vizimba | Tshs 20,000/= |
| XII. | Ujenzi wa majengo | Tshs 100,000/= |
| XIII. | Maeneo mengine ambayo hayajatajwa | Tshs 100,000/= |

**SEHEMU YA NANE**

**ADA YA USAJILI NA USHURU WA KUEGESHA VYOMBO VYA UVUVI**

| | | |
|---|---|---|
| | Ushuru wa kuegesha vyombo vya usafiri majini | Tshs 30,000/= kwa mwezi |
| | Ushuru wa kuegesha vyombo vya kigeni | Asilimia 50% ya bei ya usajili wa chombo. |
| | Ada ya usajili wa vyombo vya uvuvi | Tshs 20,000/= |

SEHEMU YA TISA

1. Viwango vya Ada za upimaji ardhi

| | | |
|---|---|---|
| | Tozo za upimaji Ardhi/Viwanja | Tsh. 2,000/= kwa kila mita ya mraba |

2. Tozo ya kuandaliwa mchoro wa Mipangomiji kulingana na ukubwa wa Ardhi:-

| | Mita ya mraba | Kiasi |
|---|---|---|
| I. | 0 - 2,000 | 100,000/= |
| II. | 2,000 - 4,047 | 200,000/= |
| III. | 4,047 - 20,235 | 250,000/= |
| IV. | 20,235 - na kuendelea | 300,000/= |

3. Tozo kwa ajili ya huduma za kubadili matumizi ya ardhi itakuwa Tshs. 300,000/= kwa kiwanja.

SEHEMU YA KUMI

I. ADA YA UHAKIKI WA MAOMBI YA VIBALI VYA UJENZI

| **NA.** | AINA YA UENDELEZAJI | KIWANGO CHA MALIPO (TSHS) |
|---|---|---|
| 1. | Majengo ya makazi | |
| | Jengo la kawaida | 50,000/= |
| | Jengo la ghorofa moja | 100,000/= |
| | Jengo la zaidi ya ghorofa moja | 200,000/= |
| | | |
| 2. | Majengo ya biashara | |
| | Jengo la kawaida | 60,000/= |
| | Jengo la ghorofa moja | 300,000/= |
| | Jengo la ghorofa mbili | 500,000/= |
| | Jengo la zaidi ya ghorofa mbili | 1,000,000/= |
| | | |
| 3. | Majengo la viwanda | |
| | Jengo la kiwanda cha kawaida | 1,000,000/= |
| | Jengo la kiwanda kikubwa | 1,500,000/= |
| | | |
| 4. | Vituo vya mafuta | |
| | Kituo cha kuuza mafuta tu (filling Station) | 500,000/= |
| | Kituo cha kuuza mafuta na kutoa huduma zingine (Service Station) | 1,000,000/= |
| | | |
| 5. | Nyumba za kupangisha (Housing Estates) | |
| | i) Nyumba ya kawaida | 60,000/= |
| | ii) Nyumba ya ghorofa moja | 300,000/= |
| | iii) Nyumba ya ghorofa mbili | 500,000/= |
| | iv) Nyumba ya zaidi ya ghorofa mbili | 1,000,000/= |
| | | |
| 6. | Majengo ya umma | |
| | v) Jengo la kawaida | 50,000/= |
| | vi) Jengo la ghorofa moja | 100,000/= |
| | vii) Jengo la ghorofa mbili | 200,000/= |
| | viii) Jengo la zaidi ya ghorofa mbili | 450,000/= |
| | | |
| 7. | Sehemu za kupumzika/burudani (Recreation Centres) | |
| | i) Maeneo ya michezo ya watoto tu | 500,000/= |
| | ii) Maeneo ya huduma mchanganyiko za burudani (kupumzika, michezo, kuongelea, n.k) | 1,000,000/= |

| | | |
|---|---|---|
| 8. | Maeneo ya maegesho | |
| | i) Maegesho ya magari madogo | 500,000/= |
| | ii) Maegesho ya magari makubwa | 1,000,000/= |
| | | |
| 9. | Maeneo ya michezo | |
| | Viwanja vya michezo | 1,500,000/= |
| | | |
| 10. | Uzio | |
| | i) Uzio maeneo ya makazi | 30,000/= |
| | ii) Uzio maeneo ya biashara | 100,000/= |
| | iii) Uzio maene ya umma | 30,000/= |
| | | |
| 11. | Mnara wa mawasiliano | |
| | Mnara wa mawasiliano | 500,000/= |
| 12 | Tenki la mafuta/gesi | |
| | i) Tenki la mafuta maeneo ya biashara | 1,500,000/= |
| | | |
| | | |
| 13 | Mnara wa tenki la maji | |
| | i) Mnara maeneo ya makazi | 20,000/= |
| | ii) Mnara maeneo ya biashara | 50,000/= |
| | iii) Mnara maeneo ya umma | 20,000/= |
| | | |
| 14 | Tenki la maji | |
| | i) Tenki la maji maeneo ya makazi | 20,000/= |
| | ii) Tenki la maji maeneo ya biashara | 50,000/= |
| | iii) Tenki la maji maeneo ya umma | 20,000/= |

Kuongeza na kubadili jengo lililopo

i). Kwa kuongeza tu 50% ya kibali cha awali

ii) Kwa kubadili 50% ya kibali cha awali

iii) Kuongeza na kubadili 100% ya kibali cha awali

II. ADA YA VIBALI VYA UJENZI

| *S/NA.* | *UKUBWA WA ENEO ($M^2$)* | *MAKAZI* | *BIASHARA/VIWANDA* | *MAJENGO YA UMMA* |
|---|---|---|---|---|
| 1. | 0 – 50$M^2$ | 50,000/= | 100,000/= | 40,000/= |
| 2. | 51 – 100 | 100,000/= | 200,000/= | 80,000/= |
| 3. | 101 – 150 | 150,000/= | 300,000/= | 120,000/= |
| 4. | 151 – 200 | 200,000/= | 400,000/= | 160,000/= |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 5. | 201 – 300 | 250,000/= | 500,000/= | 200,000/= |
| 6. | 301 – 400 | 300,000/= | 600,000/= | 240,000/= |
| 7. | 401 – 500 | 350,000/= | 700,000/= | 280,000/= |
| 8. | 501 – 600 | 400,000/= | 800,000/= | 320,000/= |
| 9. | 601 – 700 | 450,000/= | 900,000/= | 360,000/= |
| 10. | 701 – 800 | 500,000/= | 1,000,000/= | 400,000/= |
| 11. | 801 – 950 | 700,000/= | 1,500,000/= | 500,000/= |
| 12. | Ongezeko kila mita za mraba 95 | 50,000/= | 100,000/= | 40,000/= |
| 13. | Uzio kwa mita | 500/= | 1,000/= | 500/= |
| 14 | Kituo cha mafuta kwa mita ya mraba ya eneo la nje liliosakafiwa (paved area) | - | 1000/= | 300/= |
| 15 | Eneo la maegesho ya magari kwa mita ya mraba ya eneo la nje liliosakafiwa - pavement | - | 1000/= | 300/= |
| 16 | Eneo la kupumzika/burudani kwa mita ya mraba ya eneo lililoainishwa (identified) | - | 1000/= | - |
| 17 | Kiwanja cha michezo kwa mita ya mraba ya eneo la nje liliosakafiwa (paved area) | - | 1000/= | 200/= |
| 18 | Minara ya mawasiliano – kila mnara | - | 1,000,000/= | 500,000/= |
| 19 | Mabwawa yakuogelea (swimming pools) kwa mita za mraba | 3,000 | 5,000 | 2,500 |
| 20 | Matenki ya mafuta/gesi (kwa mita za ujazo) | | | |
| | 0 – 1000m$^3$ | - | 2,500,000/= | - |
| | 1001 – 2500m$^3$ | - | 4,000,000/= | - |
| | 2501 – 4000m$^3$ | - | 5,500,000/= | - |
| | 4001 – 6000m$^3$ | - | 7,000,000/= | - |
| | Ongezeko kila mita za ujazo 500 | - | 350,000/= | - |
| 21 | Minara ya matenki ya maji kwa mita ya mraba | 5,000 | 8,000/= | 4,000/= |
| 22 | Matenki ya maji (kwa kila mita 1000 za | 2,000/= | 3,000/= | 1,500/= |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 5. | 201 – 300 | 250,000/= | 500,000/= | 200,000/= |
| 6. | 301 – 400 | 300,000/= | 600,000/= | 240,000/= |
| 7. | 401 – 500 | 350,000/= | 700,000/= | 280,000/= |
| 8. | 501 – 600 | 400,000/= | 800,000/= | 320,000/= |
| 9. | 601 – 700 | 450,000/= | 900,000/= | 360,000/= |
| 10. | 701 – 800 | 500,000/= | 1,000,000/= | 400,000/= |
| 11. | 801 – 950 | 700,000/= | 1,500,000/= | 500,000/= |
| 12. | Ongezeko kila mita za mraba 95 | 50,000/= | 100,000/= | 40,000/= |
| 13. | Uzio kwa mita | 500/= | 1,000/= | 500/= |
| 14 | Kituo cha mafuta kwa mita ya mraba ya eneo la nje liliosakafiwa (paved area) | - | 1000/= | 300/= |
| 15 | Eneo la maegesho ya magari kwa mita ya mraba ya eneo la nje liliosakafiwa - pavement | - | 1000/= | 300/= |
| 16 | Eneo la kupumzika/burudani kwa mita ya mraba ya eneo lililoainishwa (identified) | - | 1000/= | - |
| 17 | Kiwanja cha michezo kwa mita ya mraba ya eneo la nje liliosakafiwa (paved area) | - | 1000/= | 200/= |
| 18 | Minara ya mawasiliano – kila mnara | - | 1,000,000/= | 500,000/= |
| 19 | Mabwawa yakuogelea (swimming pools) kwa mita za mraba | 3,000 | 5,000 | 2,500 |
| 20 | Matenki ya mafuta/gesi (kwa mita za ujazo) | | | |
| | 0 – 1000m$^3$ | - | 2,500,000/= | - |
| | 1001 – 2500m$^3$ | - | 4,000,000/= | - |
| | 2501 – 4000m$^3$ | - | 5,500,000/= | - |
| | 4001 – 6000m$^3$ | - | 7,000,000/= | - |
| | Ongezeko kila mita za ujazo 500 | - | 350,000/= | - |
| 21 | Minara ya matenki ya maji kwa mita ya mraba | 5,000 | 8,000/= | 4,000/= |
| 22 | Matenki ya maji (kwa kila mita 1000 za | 2,000/= | 3,000/= | 1,500/= |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | ujazo) | | | |
| 23. | Ukarabati mdogo (renovation) | 50,000/= | 100,000/= | 40,000/= |
| 24 | Ukarabati mkubwa | 50% ya ada zilizoorodheshwa katika jedwali hili | 75% ya ada zilizoorodheshwa katika jedwali hili | 50% ya ada zilizo orodheshwa katika jedwali hili |

- Nakala ya kibali cha ujenzi iwe inabaki katika eneo la ujenzi kwa ajili ya ukaguzi wa mara kwa mara

SEHEMU YA KUMI NA MOJA
ADA ZA MATUMIZI YA FUKWE ZA BAHARI

| | | |
|---|---|---|
| | Matumizi ya fukwe za bahari | Tshs 300,000/= kwa mwezi mmoja |

SEHEMU YA KUMI NA MBILI

USHURU WA MADINI YA UJENZI

| | | |
|---|---|---|
| I. | Gari ya ujazo wa tani 2 hadi 4 | Tshs 5,000/- kwa trip |
| II. | Gari ya ujazo wa tani 5 hadi 9 | Tshs 10,000/- kwa trip |
| III. | Gari ya ujazo wa tani 10 na kuendelea | Tshs 15,000/- kwa trip |

JEDWALI LA PILI

KUFIFILISHA KOSA

*(Chini ya kifungu cha 15)*

Mimi ..................................................wa S.L.P............................ nakiri KWA HIYARI YANGU MWENYEWE mbele ya.........................................ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya ................................ kwamba mnamo tarehe......ya Mwezi....Mwaka........nilitenda kosa la kukiri masharti ya kifungu cha .............cha Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Manispaa Kigamboni za mwaka 2018.

Kwa mamlaka aliyopewa na Mkurugenzi wa Halmashauri. Niko tayari kulipa kiasi cha Ada na Ushuru ninaodaiwa pamoja na faini.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA KWA HIYARI YANGU KWA KADIRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe................ya mwezi..............mwaka......................

Jina...............................................................Saini.............................

**Mbele ya:**

Jina……………………………..……………..

Saini…………………………………………........

Wadhifa………………………………………..

Nembo ya Halmashauri ya Manispaa Kigamboni imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Halmashauri uliofanyika mnamo tarehe 31 Januari, 2018 mbele ya:-

STEPHEN E. KATEMBA
*Mkurugenzi,*
*Halmashauri ya Manispaa Kigamboni.*

L.S

MAABAD SULEIMAN HOJA
*Mstahiki Meya*
*Halmashauri ya Manispaa Kigamboni.*

NAKUBALI

Dodoma
07 Juni, 2018.

MHE. SELEMANI S. JAFO (MB.)
*Waziri wa Nchi/OR -TAMISEMI.*